# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukuwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema na utukufu, kwa kutujaalia uhai na Afya njema, na kutuwezesha kukutana tena katika Baraza la Kumi, kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ambao ndio sababu ya sisi kusimama katika Baraza hili, nasi hatuna budi kurejesha imani kwao kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote, kwa dhamira ya kutetea maslahi yao katika Baraza hili tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, Naomba niwakumbushe wajumbe wenzangu kuwa kipindi chetu cha miaka mitano kinakimbia kwa kasi kubwa, hivyo kila mmoja wetu ajitahidi kutekeleza aliyoyaahidi na kwa pamoja tutakuwa tumemsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kukamilisha ahadi kwa wananchi waliotuchagua kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekeee nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada anazochukua katika kuendeleza sekta ya elimu nchini kwa kutoa kipaumbele katika sekta hiyo na kuimarisha miundo mbinu mbali mbali ya elimu ikiwemo kujenga majengo ya skuli za ghorofa, kuboresha maslahi ya walimu pamoja na kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

Aidha napenda kukushukuru na kukupongeza wewe **Mheshimiwa Spika,** kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi na upeo mkubwa. Ni imani yangu kwamba, utaendelea kutuongoza kwa uadilifu na ustadi wa hali ya juu kwa lengo la kuimarisha Demokrasia katika chombo hiki muhimu cha kuwatumikia wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa jitihada kubwa wanazozichukua katika kusimamia sekta ya elimu na kuhakikisha sekta hiyo inafikia lengo la mageuzi ya ubora wa elimu uliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za Kamati, jambo ambalo limepelekea

wepesi kwangu kuweza kuiongoza Kamati hii inayosimamia Wizara hii muhimu. Wajumbe wa Kamati wameweza kuijadili ipasavyo Bajeti hii na kuhoji mambo mengi ya msingi, kwa lengo la kuhakikisha fedha wanazoidhinisha katika Baraza hili, zinatumika vizuri na kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. Kwa heshima ya kipekee naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kama ifuatavyo:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani — Mwenyekiti
2. Mhe. Nassor Salim Ali — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Hussen Kombo — Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis — Mjumbe
5. Mhe. Haji Omar Kheri — Mjumbe
6. Mhe. Sulubu Kidongo Amour — Mjumbe
7. Mhe. Salma Mussa Bilal — Mjumbe
8. Mhe. Bahati Khamis Kombo — Mjumbe

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi na makatibu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu, Makatibu hao ni:

1. Ndg. Talib Enzi Talib — Katibu
2. Ndg. Bakari Makame Haji — Katibu
3. Ndg. Salha Abdulla Abdulla — Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati yetu ni kupitia na kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ilikaa na kuijadili Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, sasa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati, napenda kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo **.**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 katika sekta ya uimarishaji wa Elimu nchini. Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia mwezi April 2024, Serikali iliweza kuipatia Wizara zaidi ya asilimia 70 ya makadirio ya fedha zilizopangwa na Wizara kuweza kutekeleza Programu mbali mbali kwa mashirikinao makubwa ya wananchi na Washirika wa Maendeleo. Sambamba na ukusanyaji wa mapato kupatikana kwa asilimia 67 ya makadirio yaliyopangwa.

**Mheshimiwa spika,**

Licha ya utekelezaji huo, Kamati imebaini kuwepo changamoto mbali mbali katika utekelezaji huo ikiwa ni pamoja na Kutopatikana fedha kwa wakati kunakosababisha kuchelewa kwa Miradi kukamilika kwa wakati.

## *Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara kwa mwaka 2024/2025*

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imeridhika kuona kwamba Serikali imezingatia kutoa kipaumbele zaidi katika Sekta ya Elimu nchini na kufanya maamuzi ya kuongeza Bajeti mara dufu kwa Wizara hiyo kutoka shilingi Bilioni **457,299,603,300** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia shilingi Bilioni **830,955,702,000** kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa **asilimia 82.**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inaunga mkono vipaumbele vilivyozingatiwa katika utekelezaji wa Bajeti hiyo ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2024/2025.Vipaumbele hivyo ni pamoja na:

- *kuimarisha uongozi na usimamizi wa elimu katika ngazi zote za skuli,wilaya,mkoa na wizara*
- *kuimarisha Elimu ya Juu kwa kuongeza fursa za upatikanaji wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kuanzia ngazi ya Diploma pamoja na kujenga Majengo mapya (Kampas ya kudumu ya chuo cha IIT Madras*
- *kuimarisha matumizi ya teknologia katika kufundishia na kujifunzia kwa kuziunganisha na mkonga wa taifa taasisi za elimu*
- *na kuendelea kutekeleza mtaala mpya wa umahiri kwa elimu ya maandalizi ,msingi na sekondari .*

Hata hivyo, Kamati inashauri suala la Michezo kuwemo katika vipaumbele vya Wizara ili kwenda sambamba na muelekeo wa Serikali katika kuimarisha sekta ya michezo nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imeridhishwa na ongezeko la makadirio ya mapato kutoka Shilingi Milioni 396,396,336 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia shilingi Bilioni 1,140,703,000 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Hata hivyo Kamati inashauri Wizara kuhakikisha kuwa inaainisha vyanzo vyote vya mapato katika makadirio yaliyopangwa ili vyanzo hivyo viweze kufahamika.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza jumla ya **Programu Kuu 6** ambapo utekelezaji wake unasimamiwa na **Programu ndogo 9.**

## Programu Kuu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii katika mazingatio ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imepata ongezeko kubwa la fedha katika makadirio ya matumizi yaliyopangwa. Fedha hizo ni kutoka shilingi bilioni **131,918,709** hadi kufikia **236,293,614.** Kamati inapongeza uamuzi huo wa Serikali kwavile elimu bora ya Maandalizi itakayotolewa katika mazingira bora ya upatikanaji wa elimu inaostahiki ndio inayomjenga mwanafunzi kuwa vizuri kupata mafanikio katika hatua ya elimu ya juu. Ongezeko hilo linatokana na uendelezaji wa Miradi ya ujenzi wa skuli za ghorofa,ukarabati wa skuli

mbali mbali unguja na Pemba ,ujenzi wa nyumba za walimu pamoja na kuimarisha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia.

## Programu Kuu ya Elimu ya Juu

**Mheshimiwa spika,**

Kamati imeridhika na uamuzi wa serikali wa kuviondoa vyuo vyote vilivyounganishwa na Chuo Kikuu cha Taifa SUZA ili viweze kujitegemea na kuwa na Bajeti zao. Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Taasisi za vyuo hivyo ili kuweza kutekelezwa zoezi hilo hatua kwa hatua na hatimae vyuo hivyo viweze kufanya vizuri na vijana wetu waweze kuhitimu katika fani mbali mbali.

**Mheshimiwa spika,**

Kamati ilihoji juu ya sababu za ongezeko kubwa la kifedha za Programu kuu ya Elimu ya Juu na kuarifiwa kuwa huduma ya HK01030101 imeongezeka kutoka Bilioni **16,610,400,000** kwa mwaka fedha 2023/2024 hadi kufikia Shilingi Bilioni **110, 302,312,000** kwa mwaka 2024/2025. Kamati imearifiwa kuwa fedha hizo zimelengwa kutekeleza Mradi wa ujenzi wa Skuli ya Afya, Dahalia, Skuli ya meno na Clinic yake. Kamati inaishauri Wizara kusimamia vizuri Miradi hiyo ili iwe na ubora na iende sambamba na thamani ya Fedha.

Aidha, katika utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ubaharia, Kamati inaishauri Wizara kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo ni vyema kuwashirikisha wataalamu wa fani hiyo ili ujenzi uwendane na matakwa ya fani husika.

**Mheshimiwa spika,**

Kamati ilihoji bajeti ya matumizi iliyowekwa katika utekelezaji wa Huduma **HKOI030102** kwa Taasisi ya KIST ambayo imeongezeka kutoka Shilingi **Bilioni 9,727,200,000** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **Bilioni 36,749,866,000** mwaka 2024/2025. Hivyo Kamati iliarifiwa Huduma katika taasisi ya KIST, fedha zake zitatekeleza Mradi wa ujenzi wa majengo matatu ya Karakana, madarasa, Workshop ya Mafuta na Gesi, Hosteli ya Wanawake na kuboresha miundombinu ya sayansi na Teknologia .

**Programu Kuu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali**

**Mheshimiwa spika,**

Programu hii katika kuviendeleza vyuo vya mafunzo ya amali kwa kuvipatia vifaa vya kisasa na miundimbinu bora ili kutoa vijana wanaoweza kujiajiri na kukubalika katika soko la ajira hasa katika Sekta ya utalii. Aidha, ipo haja kwa Serikali kuipatia Wizara bajeti ya fedha iliyopangwa kwani katika mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia mwezi Aprili , Programu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali chini ya kifungu PKO1O4 ilipatiwa Asilimia 22 tu ya Bajeti hiyo.

**Programu Kuu ya Ubora wa Elimu**

**Mheshimiwa spika,**

Lengo la Programu hii ni kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu Unguja na Pemba. Makadirio ya bajeti kwa Programu Kuu ya Ubora wa Elimu kwa

mwaka wa fedha 2024/2025 ni shilingi Bilioni **48,565,662,000** kutoka shilingi Bilioni **12,495,809,000** kwa mwaka wa fedha uliopita. Kamati imeelezwa kuwa ongezeko hilo limetokana na kuwepo kwa huduma mbali mbali katika uboreshaji wa mfumo wa elimu nchini. Huduma hizo ni pamoja na kuandaa Mitaala na kuratibu uandaaji wa vitabu na vifaa vya kujifunzia na kufundishia, upimaji wa Tathmini ya elimu pamoja na huduma ya ukaguzi wa elimu.

**Mheshimiwa spika,**

Kamati inaipongeza Taasisi ya Elimu kwa kusimamia mageuzi katika sekta ya elimu hasa katika utekelezaji wa Mtaala mpya wa elimu. Ipo haja kwa Serikali kuzijengea uwezo zaidi wa kibajeti huduma zinazotolewa katika Programuu hii ili ziweze kwenda sambamba na mageuzi ya elimu yalikusudiwa.

Katika utekelezaji wa Programu hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejipanga kuwajengea uwezo zaidi walimu katika utekelezaji wa Mtaala mpya wa umahiri ili uende sambamba na uboreshaji wa huduma ya elimu. Hata hivyo , Wizara kuweka mkazo zaidi katika kuzipitia Skuli binafsi na kuhakikisha kuwa zinafuata taratibu na sheria zilizowekwa katika kutoa elimu bora.

**Mheshimiwa spika,**

Kamati pia inaishauri Wizara kuzingatia Bajeti ya utekelezaji wa huduma za elimu mjumuisho na stadi za Maisha **HKOI050106**. Kamati imeona kuwa kifungu hicho bado kinahitaji mazingatio kutokana na mahitaji yanayotumika hususan kwa Watoto wenye mahitaji maalum, kama tunavyofahamu vifaa na mahitaji yao huwa na gharama kubwa. Hata hivyo

Kamati inaikumbusha wizara ya Fedha kuhakikisha kifungu cha Huduma hizi kinapatiwa fedha kwa wakati ili kuweza kusaidia vijana wetu wenye mahitaji maalum ukizingatia kuwa hadi mwezi April 2024 kitengo hicho kiliweza kupatiwa asilimia 49 ya fedha zilizopangwa.

### Programu ndogo ya Utawala na uendeshaji

**Mheshimiwa spika,**

Kamati inampongeza Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussien Ali Mwinyi kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Posho ya nauli kwa Watumishi wa umma. Kamati inaunga mkono hatua hiyo ambapo katika sekta ya Elimu itasaidia sana kuwawezesha walimu kufaidika na posho hiyo na kufanya kazi kwa ufanisi.

### Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inasimamia vizuri matumizi ya fedha za Miradi zilizopangwa katika mwaka mpya wa fedha 2024/2025. Uzoefu unaonyesha kuwa katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya ujenzi wa skuli katika bajeti 2023/2024, kumejitokeza kuongeza kwa gharama zaidi za ujenzi kinyume na makubaliano ya awali hali ambayo inapelekea Serikali kutumia fedha nyingi za ziada katika kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inaishauri Wizara kuwepo wataalamu katika ofisi ya Mipango kuhakikisha kuwa Miradi inatekelezwa kwa mujibu wa thamani ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kupitia SUZA kuendelea kutekeleza Mradi mkubwa wa Elimu ya juu kwa Mageuzi ya kiuchumi, Mradi wa (HEET) katika mwaka wa fedha 2024/2025, Mradi ambao unaotekelezwa kwa pamoja na SMT ambapo SUZA imetengewa Dola za kimarekani Milioni 8.9 ikiwa sawa na Tanzania Shilingi Bilioni 20 katika utekelezaji wa Mradi huu.

.

**Mheshimiwa Spika,**

Mradi huu umelenga kutekeleza:Ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa, jengo la Lab Complex na jengo la Skuli ya Kilimo na kuboresha miundo mbinu ya Tehama na Mitaala mipya . Kamati inaishauri Wizara kutekeleza Mradi huo kwa mujibu wa vipaumbele vilivyowekwa katika muelekeo wa mageuzi ya sekta ya elimu nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha Hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe

wa Baraza lako waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba Kamati yangu naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

……………………………………

Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

**<u>Zanzibar.</u>**